**336/1**
**LUGHA YA KISWAHILI**
**Karatasi ya Kwanza**
**Saa 2 Dakika 30**

# STANDARD HIGH SCHOOL ZZANA

**Uganda Certificate of Education**

**MID TERM ONE EXAMINATIONS 2020**

LUGHA YA KISWAHILI

**Karatasi ya Kwanza**

**Muda: Saa Mbili na Nusu**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**

*Jibu maswali manne kwa ujumla.*

*Swali la kwanza na la pili ni ya lazima*

*Kwa swali la kwanza mtahiniwa achague AMA (a) AU (b) na si zote*

***FORWARD SCANNED ANSWERS TO stahiza2020@gmail.com***

**Pindua**

**SEHEMU A**

1. **AMA**

(a) Andika insha moja ya maneno yasiyozidi 450 wala kupungua 350 kuhusu moja ya mada (vichwa) zifuatazo;

(alama 40)

(i) Kuuliza si ujinga

(ii) Hadithi ya babu

(iii) Safari ya Jumada kuelekea Namugongo

(iv) ……………………………. nilikubali kwaamba tajiri hana utu

**AU**

(b) **Andika insha mbili kila yenye maneno yasiyozidi 250 wala kupungua 180.** (alama 40)

(i) Wewe ni mgombea Urais wa nchi Uganda. Mwaka ni 2021 na siku ni ya mwisho wa kampeni na umepiga kambi katika wilaya ya Kampala. Andika hotuba utakayowatolea wanakampala.

(ii) Kuna nafasi ya kazi imetangazwa katika gazeti moja la kienyeji "Orumuri" nchini Uganda. Shule ya upili ya Falkoni inahitaji huduma za mwalimu wa somo la Kemia aliye na umri usiozidi 30. Andika barua kwa mwalimu mkuu wa hiyo shule ukiiomba kazi.

(iii) Kwa kikao ulichohudhuria shuleni kwako, chukulia kuwa wewe ni karani. Andika kumbukumbu za mkutano huo

(iv) Andaa resipe ya ugali na nyama kwa watu watatu.

## SEHEMU B

2. **Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yaliyoulizwa.**

Kati ya viumbe vyote vilivyoumbwa na Rabana, binadamu ndiye aliyetunukiwa uwezo mkubwa wa akili zaidi. Huwezi ukafananisha kiwango cha uwezo wa ubongo wa binadamu na cha kiumbe kingine kile. Hata inasemekana kuwa Mola alimwumba binadamu kwa mfano wake mwenyewe. Ninao uhakika kuwa Mumba alifanya hayo akiwa na matumaini kwamba mwanadamu angeutumia uwezo huo kwa njia inayofaa. Angeutumia uwezo huo kufanya tafakuri na taamuli inayofaa. Angeutumia kuhudumia viumbe vingine ifaavyo, kuishi kwa amani na binadamu mwenziwe bila kuzusha tafiri na tafishi, kuhifadhi na kuimarisha rai yake na hata kufurahia maisha

Akiwa na uwezo huo wote ulimwenguni, ingetarajiwa binadamu aridhike. Kwa bahati mbaya, mambo sivyo hivyo. Iwapo kuna kiumbe ambacho hakijaridhika kamwe, si kingine bali ni binadamu. Hili linadhihirishwa wazi na mambo anayoyafanya hapa duniani.

Utashangaa na labda uduwae nikukueleza kwamba binadamu haridhiki hata kwa maumbile yake. Ni wangapi ushawaona wakijaribu kubadilisha rangi ya ngozi zao? Wanazichoma nywele eti ziwe laini, kucha zinapakwa rangi, kope na nyusi zinanyolewa au kupakwa rangi. Wengine wametia mapambo karibu na kila kiumbe cha mwili. Sikioni ni herini, usoni ni chale, mikononi ni bangili na midomoni ni ndunya. Ukiwaona wengine utadhani wametumbukiza midomo yao damuni. Lo! Yapi haya! Kwa nini tufanye hayo yote iwapo tumeridhika?

Mambo ya mavazi ni yayo hayo. Kila mtu huvaa kwa njia anayofikiria inamridhisha. Wengi hubadilisha mitindo ya mavazi kila wakati eti wakitafuta kuridhika. Leo utawaona na mavazi makubwa kupita kimo chao. Kesho utawaona na mengine yanayowabana na mafupi kupita kiasi. Usishangae ukiwaona kesho kutwa wakiwa rabana. Yote hayoo eti kwa kutafuta kuridhika.

Leo hii utamwona binadamu akilia kwa kukosa mtoto. Utasikia kwenye vyombo vya habari wengine wakifikishwa mahakamani kwa majaribio ya kuwaiba watoto wa wengine. Wakati uo huo utawasikia wengine wakifikishwa kortini kwa hatia ya kuzaa na kuwatupa watoto wao. Si hayo tu, utamwona mtu akiendelea kujifungua watoto mwaka baada ya mwaka eti anataka mtoto mvulana. Ubwege upi huu? Tutaelewa lini kuwa mtoto ni mtoto na mtoto msichana ni sawa na mtoto mvulana?

Mambo ya mali na vyeo ni yayo hayo. Kamwe sisemi mtu asiwe na malengo ya juu. La hasha! Lakini ukweli ni kwamba binadamu haridhiki kwa mali na vyeo. Chifu anataka kuwa mkuu wa tarafa, mkuu wa tarafa anataka kuwa mudiri naye mudiri anatamani hata kuwa rais. Kumbuka hata kunao wanaotaka kuwa Mungu. Mungu wangu tunusuru!

Utawasikia wengine wakinung'unika na kulalamika eti wamekosa wapenzi. Wakati uo huo, utawaona wengine wakifikishana mbele ya hakimu wakitaka kuzitupilia mbali ndoa zao. Kamwe wameshindwa kuridhika katika maisha ya ndoa. Wanaume wengine wanaoa hata wake zaidi ya mmoja eti bado hawajaridhika. Wanawake nao ni vivyo hivyo, wanataliki mwanamume mmoja na kuolewa na mwingine. Uzinzi umekita mizizi kwa sababu wahusika hawajaridhika na wenzao. Aibu kubwa. Shtuka na ujihadhari usizimie nikikueleza kuwa wapo binadamu ambao hawaridhiki kimapenzi na binadamu wenzao. Badala yake wametafuta 'mapenzi ya kuridhisha' kwa wanyama. Utamwona binadamu anayedai kuwa na akili timamu akimfanya ng'ombe au mbuzi 'mke wake'! wanyama kama vile kuku, mbwa na kima hawajabahatika kunusurikawimbi hili. Haya hata yana aibu kuyataja. Hata hivyo lazima niyataje kwani ukimstahi mke ndugu huzai naye.

Ni mengi yanayotendwa na binadamu ambayo ni dhihirisho tosha kuwa hajaridhika. Swali ni hili, ataridhika lini iwapo kweli shani itatokea aridhike?

**Maswali:**

(a) Pendekeza kichwa cha taarifa hiyo. (alama 02)

(b) Ipi tofauti kubwa sana kati ya binadamu na viumbe wengine? (alama 02)

(c) Ni jambo gani linalodhihirisha kuwa binadamu haridhiki na uzuri wa sura yake? (alama 02)

(d) Ni yapi maoni ya mwandishi kuhusu mtoto msichana na mtoto mvulana? (alama 02)

(e) Tabia ya uzinzi inasababishwa na nini? (alama 02)

(f) Eleza jinsi binadamu haridhiki kwa mali na vyeo kulingana na taarifa. (alama 03)

(g) Je, unafikiri kwamba mwandishi amefurahia au amechukizwa na matendo ya binadamu? Toa sababu zako. (alama 05)

(h) Mwandishi anamaanisha nini akisema kuwa wanyama kama vile kuku, mbwa na kima hawajabahatika kunusurika wimbi hili? (alama 02)

3. **Fupisha habari kwa maneno themanini (80)** (alama 20)

**UKIMWI**

UKIMWI ni mojawapo ya magonjwa ya zinaa kama vile kisonono, kaswende na vidonda kwenye sehemu za siri za mtu. Ugonjwa wa UKIMWI ni hatari sana kwa sababu unafanya mwili kuwa dhaifu kutokana na virusi vyake kuharibu chembe nyeupe za damu mwilini ambazo kazi yake ni ulinzi dhidi ya virusi vinavyosababisha magonjwa mwilini.

Mara tu virusi vya UKIMWI viingiapo mwilini, huanza kuharibu zile chembe za damu za ulinzi kuzifanya chembe hizo kutotimiza wajibu wake wa kulinda mwili ili mtu asipate magonjwa. Sasa mwili huwa dhaifu sana kiasi kwamba mtu anayeugua ugonjwa wa UKIMWI hukumbwa na magonjwa ya kila aina. Hiyo ndiyo sababu ugonjwa huu unajulikana kwa jina la UKIMWI ambalo jina hili ni ufupisho wa ‘ukosefu wa kinga mwilini’.

Ugonjwa wa UKIMWI ni hatari mno kuliko ugonjwa wowote ulimwenguni sasa hivi kwa sababu hakuna dawa ya kutibu ugonjwa huu kwa sasa. Tena, ugonjwa huu ni hatari sana kwani virusi vyake vinaweza kujificha katika mwili wa binadamu kwa muda mrefu bila mtu huyo kuonyesha dalili za ugonjwa. Kwa muda huo, mtu huyo anaweza kuambukiza ugonjwa huo kwa watu wengine kwani si rahisi kutambua kwamba mtu huyo ni mgonjwa.

Sasa hivi, njia kuu ya kusambaza virusi vya UKIMWI kutoka mtu hadi mwingine husemwa kwamba ni kupitia kwa kitendo cha kuzini. Kuna njia nyinginezo ambazo kwazo UKIMWI huambukizwa nazo ni kutoa damu kwa mgonjwa, kutumia sindano ile ile kwa wagonjwa mbalimbali hospitalini wakati wa kudungwa sindano na kukata kucha au sehemu nyingine za mwili kwa kutumia wembe mmoja kwa watu wengi.

4. **Jibu maswali ya sarufi yafuatayo:**

(A). Kanusha amri zifuatazo*:*

(a) Fanyeni! (alama 01)

(b) Kimbieni! (alama 01)

(c) Soma! (alama 01)

(B). Jaza mapengo katika sentensi zifuatazo ukitumia viwakilishi mwafaka.

(a) Vijana _nahitaji michezo. (alama 01)

(b) Kulala mchana _takufanya mzembe (alama 01)

(c) Miti _likatwa juzi (alama 01)

(C). Andika sentensi zifuatazo ili ziwe katika lugha inayokubalika kisahihi.

(a) Maembe tatu zinatosha (alama 01)

(b) Mama anapikanga chakula mzuri (alama 01)

(D). Ziandike sentensi zifuatazo kwa usemi taarifa.

(a) "Sasa mmeanza kuongea vibaya," alisema mwenzao. (alama 01)

(b) "Leo ni siku yangu ya mazaliwa," Salah alitukumbusha. (alama 01)

(E). Unganisha hizi sentensi kwa kutumia viunganishi katika mabano:

(a) Tuliona watoto wanene. Watoto walikuwa wazuri. (--- ambao ---) (alama 01)

(b) Nilichelewa kupata chakula. Nilipoteza sahani yangu. (--- kwa sababu --) (alama 01)

(F). Tunga sentensi mbili mbili za haya maneno kuonyesha kuwa unajua maana tofauti

(a) Nyanya (alama 01)

(b) Vua (alama 01)

(G). Andika wingi wa sentensi zifuatazo*:*

(a) Baiskeli ya baba yangu imeharibika. (alama 01)

(b) Kinyozi atapigiwa simu leo. (alama 01)

(H). Tunga sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi hivi:

(a) Juta (alama 01)

(b) Fitini (alama 01)

(I) Toa kinyume cha haya maneno*:*

(a) Umba (alama 01)

(b) Fuma (alama 01)

5. **Tafsiri habari ifuatayo kwa Kiswahili.** (alama 20)

When the soldiers arrived at my office, they told me that I was under arrest and that, if I tried to play my monkey tricks, they would shoot me at once. They even demanded to know why I had not gone to the workshop to wait for and welcome *affande*, their boss. Didn't I know that he was going there to take delivery of the new special car? Was I not the one who had personally invited the boss to go to the workshop? How could I dare to be so rude and disobedient? Didn't I know that the boss was a senior army officer and the chairman of the Miltary Tribunal who could indefinitely shut the workshop and lock me up or worse for my insubordination? With those threatening questions, the soldiers immediately took me to the workshop to join my already kneeling staff, and face Col. Butabika's music.

When I was produced at the workshop by the two soldiers who had come for me from my Udyam House office, I found the colonel standing before the kneeling Spear Motors garage staff, brandishing two pistols and hysterically haranguing his victims in a mixture of Kiswahili and his native Nubian language. As soon as he saw me, he seemed to lose his senses. The colonel immediately turned all his wrath on me. 'You are a dangerous man to my life and you are no different from the guerrillas from Tanzania who are fighting the government', he accused me.

*From: Gordon B.K Wavamunno*
*The story of an African Entrepreneur*

**MWISHO**